

# KISWAHILI KIDATO CHA TATU

102/3

## KISWAHILI

### KARATASI YA TATU

(FASIHI)

MUDA:SAA 2 ½

#### MAAGIZO

- Jibu maswali manne pekee
- Swali la kwanza ni la lazima
- Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja
- Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu zilizobaki.
- Mtahiniwa ahakikishe kuwa maswali yote yamo.

#### KWA MATUMIZI YA MTAHINIWA PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
SEHEMU A	20	
SEHEMU B	20	
SEHEMU C	20	
SEHEMU D	20	
SEHEMU E	20	
JUMLA	80	

## 5. USHAIRI

### Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuatia

Mwenye nacho wajishasha, wajiona kama ndovu  
Kitu kimekuleweshwa, huutambuwi uwovu  
Ngoma yako itakesha, au ni nguvu za povu?  
Tangu lini muwerevu, akajinyowa mwenyewe?

Tangu ukipate kitu, 'megeuka mpumbavu  
Kattu huthamini mtu, ambaye kwamba mtovu  
Wafikiri kisu gutu, hakikati nyama pevuvu?  
Tangu lini muwerevu, akajinyowa mwenyewe?

Wangapi 'meonekana, mibakhili mishupavu  
Waliyo wakijitona, na mwingi usuluhivu  
Leo hawanasi tena, wageukile maivu,  
Tangu lini muwerevu, akajinyowa mwenyewe?

Kupata kusikughuri, ukajidhani mwerevu  
Na hicho chako kiburi, ujuwe ni maangavu  
Iko siku itajiri, ujikute mwenye wavu  
Tangu lini muwerevu, akajinyowa mwenyewe?

Kila mwenye kukuonya, uiwate ndiya mbovu  
Huchelewi kumminya, kumvunda zake mbavu  
Fanya ambayo wafanya, hutajinyowa mwenyewe  
Ungajidai mwerevu, hutajinyowa mwenyewe

(Kutoka kwa, Sauti ya Dhiki, uk. 9, Abdilatif Abdalla, O.U.P.)

### Maswali

1. Lipe shairi hili kichwa mwafaka. (alama 1)
2. Pambanua umbo la shairi hili (alama 4)
3. Taja na kufafanua maudhui mawili yanayojitokeza katika ubeti wa kwanza. (alama 3)
4. Dhihirisha tamathali ya usemi iliyotumiwa katika mleo wa ubeti wa pili. (alama 2)
5. Dhihirisha uhuru wa ushairi. (alama 4)
6. Uandike ubeti wa nne kwa lugha ya nathari. (alama 3)
7. Eleza maana za maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi: (alama 3)
  - (i) kitu
  - (ii) mtovu
  - (iii) kusikughuri

**SEHEMU B:RIWAYA-KIDAGAA KIMEMWOZEA(KEN WALIBORA)**

2.Anwani kidagaa kimemwozea inaafiki riwaya hii. Thibitisha (alama 20)

**AU**

3.“Alijifungia mle chumbani akaketi kitandani na kuanza kusoma tena ile barua huku miguu na mikono inamtetema na mtima kudunda.”

- a. Eleza muktadha wa usemi huu (alama4)
- b. Eleza ujumbe uliojiri katika barua iliyosomwa na mhusika huyu(alama 8)
- c. Jadili sifa za mwandishi wa barua hii(alama 4)
- d. Taja barua zingine nne zilizoandikwa katika riwaya hii.(alama4)

**SEHEMU C: TAMTHILIA-Mstahiki Meya-T.Arege**

4.Fafanua uozo wa kijamii unaojitokeza katika tamthilia ya mtahiki meya(alama 20)

**AU**

5.“Hata Bwana aliteswa kwa sababu ya neno.Mateso yake yalikuwa makubwa.Hayawezi kulinganishwa na tendo hili dogo.Walifanya vizuri kuja.”

- a. Eleza muktadha wa dondoo hili(alama 4)
- b. Eleza sifa za mzungumzaji(alama6)
- c. Fafanua aina tano ya mogogoro inayojitokezea katika tamthilia ya mstahiki meya(alama10)

**SEHEMU D**

**HADITHI FUPI-DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE**

**(ken walibora na S.A Mohamed).**

**DAMU NYEUSI- KEN WALIBORA**

Eleza jinsi ubaguzi na unyanyasaji unavyojitokeza katika hadithi hii.(alama20)

**AU**

7.“Leo ni siku ya siku ,siku ya nyani kufa ambapo miti yote huteleza.”

- a. Eleza muktadha wa dondoo hili.(alama4)
- b. Tambua tamthilia za usemi zilizotumika katika dondoo hili.(alama4)

- c. Huku ukitoa mifano thibitisha maudhui ambayo yamejitokeza katika Hadithi ya Damu Nyeusi.(alama20)

## **SEHEMU E**

### **FASIHI SIMULIZI**

- a. Misimu ni nini?(a12)
- b. Tofautisha visasili na visakale(a14)
- c. Fafanua sifa nne za mighani(a14)
- d. Eleza majukumu matano ya ngano katika jamii(a15)
- e. Jadili matatizo yanayokabili fasihi simulizi katika jamii ya sasa(a15)